

UFALME WA MBINGUNI

“Siku zile aliondokea Yohana Mbatizaji akihubiri katika nyika ya Uyahudi, na kusema, Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.” Mathayo 3:1-2.

“Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, Yesu akaenda Galilaya, akihubiri Habari Njema ya Mungu, akisema, Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini injili” Marko 1:15..

“Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele.” Danieli 2:44.

“Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa wanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbinguni akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye. Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wantumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo hayatapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa.” Danieli 7:13-14.

“Malaika wa saba akapiga baragumu, pakawa na sauti kuu katika mbingu; zikisema, Ufalme wa dunia umekwishakuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atamiliki milele na milele.” Ufunuo 11:15.

UFALME WA MBINGUNI

Toleo la kwanza;
April, 2013

Kitabu hiki hakiuzwi. Kinatolewa bure kwa watu wote na wa mahali popote pale {soma Mathayo 10:7-9}. Kitabu hiki ni sauti ya Mungu inayonena na watu wake kupitia Maandiko Matakatifu, yaani Biblia.

Uchapaji wa kitabu hiki huwezesha na fungu la kumi la waumini wa Kanisa la Mungu pamoja na michango ya hiyari kutoka kwa wasomaji wetu. Wewe pia waweza kushiriki mbaraka huu mkubwa kwa hiyari yako mwenyewe kuchangia kazi hii ya utume kuwafikia walengwa kwa kutoa mchango wako; naye Mungu wa mbinguni atakujazi fadhili zake za milele. 2 Wakorintho 9:6-8.

Pia kitabu hiki hakiegemei dhehebu lo lote lile katika mafundisho yake; bali kinafundisha na kuweka wazi kweli ya biblia pekee; ni hazina iliyositirika, kimejaa siri za ufalme wa mbinguni. Na kikiishakukujulisha kweli ya biblia; ndipo hiyo kweli yenyewe itakapokuweka huru kweli. Yohana 8:31-32.
Hebu jipe moyo mkuu, ukisome kitabu hiki, kwani ni mbaraka mkubwa uliokujilia leo hii.

Haki zote zimehifadhiwa

UTANGULIZI.....	1
Sura ya kwanza.....	2
HAPO MWANZO.....	2
Sura ya pili.....	3
KUUMBWA KWA MWANADAMU.....	3
Hatua tatu za uumbwaji wa Mwanadamu.....	3
Sura ya tatu.....	4
WOKOVU.....	4
Awamu ya kwanza ya wokovu.....	4
Ujio wa Kristo mara ya kwanza.....	5
Toba na msamaha.....	6
Sura ya nne.....	7
UJIO WA KRISTO MARA YA PILI.....	7
Vita vya mwisho.....	7
Ufufuo wa kwanza.....	8
Ufalme wa mbinguni warejeshwa duniani.....	9
Wafalme na Makuhani wa Mungu.....	9
Ulimwengu wa Amani tele.....	10
Kuponywa madhara ya dhambi.....	11
Kufunguliwa kwa Shetani.....	11
Sura ya tano.....	12
AWAMU YA TATU YA WOKOVU.....	12
Uzima wa milele kutolewa kwa wote.....	12
Ufufuo wa pili kwa nafasi ya wokovu.....	12
Kiti cha enzi kikubwa cheupe cha hukumu.....	13
Ni nini hatima ya wote wanaokataa kutubu?.....	15
Sura ya sita.....	16
YERUSALEMU MPYA.....	16
Sura ya saba.....	17
VIPI KUHUSU KWENDA MBINGUNI?.....	17
Dhana dhidi ya ukweli.....	17
Mfano hai.....	18
Je! Watakatifu wanaokufa wanakwenda mbinguni?.....	19
Hitimisho.....	20

UTANGULIZI

Wapendwa; tunaishi katika ulimwengu uliojawa na kila aina ya shida, dhiki, taabu na misiba mbalimbali. Na kila mwanadamu katika ulimwengu huu; kwamba ni mtoto au kijana, mtu mzima au mzee, wote tunaguswa na dhiki hizi za dunia hii. Vita vya kila aina; yaani vita kuanzia katika familia, ukoo, kabila, taifa na hata vile vya kimataifa vimeshuhudiwa karibu na kila mmoja wetu. Je, kuna mtu anayefurahishwa na maisha hayo ya vita? Na je, ni kwa nini vita vinaendelea kutokea na kuongezeka duniani kila kunapokucha; ni nini chanzo chake?

Hata hivyo pia, tunaishi katika ulimwengu uliojawa na kila aina ya magonjwa; makubwa kwa madogo, yatishayo pamoja na yale tuyaonayo kuwa ya kawaida, tena kila kunapokucha magonjwa mengine mengi sana yanazidi kuongezeka na kujitokeza. Na hakuna binadamu asiyeguswa na magonjwa haya, na badala yake wote tunasumbuliwa na kuteswa na magonjwa hayo ambayo yamewaua wenzetu wengi sana na kila siku yanaendelea kuua. Je, yupo mtu anayependezwa na magonjwa hayo? Na je, ni nini chanzo cha magonjwa hayo?

Pamoja na hayo bado pia tunaendelea kushuhudia majanga madogo kwa makubwa yanayotisha ambayo yanaendelea kuteketeza maisha ya maelfu elfu ya watu kila siku. Majanga hayo ni pamoja na matetemeko ya ardhi, vimbunga, sunami, ukame, mafuriko, ajali za kila mahali; yaani ajali za barabarani, majini, angani pamoja na majanga mengine mengi kama hayo. Je, kuna mtu anayefurahishwa na majanga hayo ya hatari? Je, ni nini chanzo cha majanga hayo?

Leo katika ulimwengu huu yapo mashirika mengi yaliyoanzishwa kwa malengo na madhumuni ya kukabiliana na hali hizi zote ili mwanadamu aweze kuishi maisha ya raha. Yapo mashirika ya afya duniani kwa ajili ya kutokomeza magonjwa yote duniani; lakini je, wanafaulu? Ukweli ni kwamba kadiri wanavyojaribu kupambana na magonjwa, ndivyo na magonjwa yanavyozidi kuongezeka kwa kasi zaidi; sasa basi, tunaelekea wapi?

Bila kusahau pia, yapo mabaraza ya usalama mengi na hata yale ya umoja wa mataifa kwa kusudi la kuzuia vurugu, ugaidi na vita vya kila aina duniani. Cha kushangaza ni kwamba, pamoja na mabaraza hayo kufanya kazi usiku na mchana; lakini badala yake kila kunapokucha ndivyo uovu, ugaidi na vita vinaendelea kutokea huku na kule duniani. Je, ipo siku mabaraza hayo yatafaulu kutokomeza ugaidi na vita duniani, ama tunaelekea wapi?

Hali kadhalika mashirika ya kupambana na majanga nayo yapo mengi sana, lakini nayo pia yameshindwa kuzuia na kumaliza majanga; na badala yake kila siku majanga yanaongezeka hapa na pale duniani. Wafalme, maraisi na viongozi wakubwa wa dunia pamoja na Wanasayansi wanaendelea kuumiza vichwa vyao kila siku kwa kuona jinsi jitihada zao za kuiboresha dunia kuwa mahali salama pa kuishi zinavyogonga mwamba. Sasa je! Tunatarajia kuiona dunia katika sura ya namna gani miaka kadhaa ijayo? Wakati maadili nayo yakizidi kuporomoka, na matukio pamoja na visa vya ajabu vikiripotiwa kila siku; je, ni nini hatima ya ulimwengu?

Ni kwa nini Mungu aliiumba dunia hii? Je, maisha haya ya taabu na yaliyo mafupi ndiyo yale yaliyokusudiwa na Mungu kwamba mwanadamu aishi kwayo ama ni nini chanzo chake? Kutokana na hali mbaya na ya hatari ya ulimwengu, je; Mungu muumbaji ana makusudi gani na maisha ya mwanadamu? Je, Mungu ana mpango wa kuiangamiza kabisa dunia isiwepo tena, ama ana mpango wa kuifanya kuwa mahali salama pa kuishi nani kwa ajili ya nani hasa?

Wapendwa; baada ya dhiki ni faraja. Kitabu hiki, “**UFALME WA MBINGUNI**”, kupitia BIBLIA TAKATIFU, kina habari njema kwako na kwa ulimwengu wote pia. Je; ni habari gani hizo njema katika ulimwengu unaozidi kukumbwa na matatizo makubwa katika nyanja zote? **Naam; Ni Habari Njema za Ujio wa Ufalme wa mbinguni hapa Duniani.** Ni ufalme ulioahidiwa na Mungu tangu zamani kupitia kwa vinywa vya Manabii wake Watakatifu, na ukahubiriwa na Yesu Kristo

pamoja na Mitume wake; tena akaliagiza Kanisa lake kuihubiri habari hiyo hata wakati huo uliokusudiwa utakapowadia; nasi Kanisa la Mungu, tunatimiza jukumu tulilopewa.

Sasa basi; tunakushauri kukisoma kitabu hiki kwa umakini sana ukiwa na Biblia yako kufuatilia kila kipengele ili ukatambue makusudi ya Mungu kuhusu maisha yako na ulimwengu kwa ujumla. Mungu wa neema yote na awape roho ya ufahamu katika kuyajua mapenzi yake na makusudi yake kupitia kitabu hiki kinachoweka wazi ukweli wa Biblia; Amina.

Sura ya kwanza

HAPO MWANZO

“Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi” Mwanzo 1:1. Naye Mungu alipoiumba nchi hii {yaani Dunia hii}, aliiumba katika namna nzuri na ya kupendeza sana, kitendo ambacho kiliwafanya Malaika kufurahi na kushangilia sana kutokana na uzuri usioelezeka wa sura ya dunia {soma Ayubu 38:7}. Na baada ya Mungu kukamilisha uumbaji wa dunia, aliiweka chini ya uongozi na utawala wa Malaika wake Watakatifu. Kwa hivyo, dunia ikawa ni sehemu ya ufalme ama utawala wa Mungu wa mbinguni usio na mipaka. Na mambo haya yalifanyika zamani sana kabla ya Mwanadamu kuumbwa.

Lakini baadaye; Malaika hao walimwasi Mungu na wakakusudia kufanya mapinduzi ya utawala kuanzia hapa duniani walipowekwa hadi juu mbinguni kwa Mungu muumba wao. Harakati hizo za mapinduzi zilipangwa na kuongozwa na Malaika Mkuu aliyelitwa Lusifa {maana ya Lusifa ni mleta nuru ama nyota ya asubuhi} ambaye alifanikiwa kuwashawishi malaika wenzake na kuungana naye katika mapinduzi hayo. Nabii Ezekieli anaeleza jinsi ambavyo uasi huo ulianza akifafanua kwa jinsi ya mithali na mafumbo {soma Ezekieli 28:11-19}.

Mungu kupitia kwa nabii Ezekieli anamzungumzia huyo malaika mkuu aliyelitwa Lusifa akisema; **“Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye; nami nalikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu {katika unabii wa biblia, mlima unamaanisha ufalme}, umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto. Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako” Ezekieli 28:14-15.**

Ni uovu gani huo ulioonekana ndani ya huyo Lusifa? Nabii Isaya anaeleza huo uovu wa Lusifa akisema; **“Nawe {yaani huyo Lusifa} ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu {nyota katika unabii wa biblia, humaanisha malaika}; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini. Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu {ama, nitafanana na Mungu}” Isaya 14:13-14.**

Harakati hizo za Shetani hazikuzaa matunda mazuri; maana tangu hapo uovu huo ulipoonekana ndani yake, Mungu alimwondoa asiwe tena mmoja wa watawala wa ufalme wake. Ezekieli anaeleza tena; **“...nawe {Lusifa} umetenda dhambi; kwa sababu hiyo nimekutoa kwa nguvu katika mlima {ufalme} wa Mungu, kama kitu kilicho najisi; nami nimekuangamiza Ewe kerubi ufunukaye, utoke katika mawe hayo ya moto” Ezekieli 28:16.** Utagundua hapa kwamba, baada ya Lusifa kuwaza uovu na kufanya uasi dhidi ya Mungu na hata kuongoza harakati za mapinduzi, jina lake likabadilika kutoka Lusifa lenye maana ya **“mleta nuru”** au **“nyota ya asubuhi”** na kuwa **“nyoka”** au **“joka”**, tena, **“Ibilisi”** na **“Shetani”**, {majina haya, **Ibilisi na Shetani**, yana maana ya **“mwaribifu”** au **“muuaji”**}, soma **Mwanzo 3:1; Ufunuo 12:9; Yohana 8:44.**

Kutokana na uasi huo; Mungu aliuondoa ufalme wake hapa duniani. Na kwa sababu hiyo basi; **“Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu {ukiwa na utupu kutokana na uharibifu wa Shetani}, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji {giza kwa sababu nuru na utukufu wa ufalme wa Mungu umetoweka duniani}” Mwanzo 1:2.**

Na kuanzia hapo, Mungu aliwaacha hao malaika waasi waendeleo kuitawala dunia kwa njia zao wenyewe; Shetani akiwa ndiye Mkuu na Mfalme wake, na hao malaika zake ndio ambao wanaitwa Pepo waovu ama Mashetani, na ndio wanaoitawala dunia hii hadi leo *{soma Waefeso 2:2-3; 6:12-13; Yohana 14:30}*. *{kwa maelezo zaidi kuhusu Shetani; agiza ujumbe wetu usemao, "SHETANI NI NANI", ama usemao, "JE! KWELI SHETANI YUPO", ili ujifunze zaidi}*

Sura ya pili

KUUMBWA KWA MWANADAMU

Baada ya hayo, Mungu alikusudia kuurejesha tena ufalme wake hapa duniani. Na hivyo basi, akadhamiria kumuumba Mwanadamu ili kupitia kwa Mwanadamu huyo aweze kuitawala tena dunia. Ndipo Mungu akaanza kuirekebisha tena dunia ambayo ilikuwa imeharibiwa na Shetani na malaika zake. Zoezi hilo la kuirekebisha *{kuifanyia maboresho}* dunia lilichukua muda wa siku sita *{soma Mwanzo 1:3-31}*. Na katika siku hiyo ya sita ya marekebisho ya dunia ndiyo ambayo Mungu alimuumba Mwandamu.

Katika kitabu hiki cha *Mwanzo 1:26* tunakuta maelezo haya; *"Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi"*.

Malengo ya Mungu hapa ni kumuumba mtu ili mtu huyo aweze kuitawala dunia yote pamoja na vyote vilivyomo ndani yake, chini ya uongozi *{mamlaka}* wa Mungu mwenyewe. Lakini kabla mtu huyo hajaitawala dunia, ni lazima aumbike na kuwa kama Mungu mwenyewe, yaani katika mfano *{maumbile}* na sura *{tabia}* ya Mungu. Na katika kitabu hiki cha *Mwanzo 1:27*, tunaona kwamba, Mwanadamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu peke yake na wala si kwa sura ya Mungu, maana anasema; *"Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimuumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba"*. Jambo hili lina maana gani? Twende pamoja tafadhalini!

Hatua tatu za uumbwaji wa Mwanadamu

Uumbwaji wa Mwanadamu unapitia katika hatua kuu tatu. Hatua ya kwanza ni kuumbwa katika mwili wa damu na nyama, yaani katika hali hii tuliyo hivi sasa. Hatua ya pili ni kupewa na kujenga ufahamu, yaani akili na tabia. Na hatua ya tatu ni kubadilishwa kuwa kiumbe wa kiroho. Kumbuka kwamba, ili mwanadamu aweze kuitawala dunia, ni lazima aumbike na kuwa kama Mungu mwenyewe. Hii ina maana kwamba, lazima afanyike kwa mfano wa Mungu na kwa sura ya Mungu pia. Lakini mpaka sasa, Mwanadamu ameumbwa kwa mfano wa Mungu pekee, na bado hajaumbwa kwa sura ya Mungu kama tulivyoona katika *Mwanzo 1:27*.

Biblia inapozungumzia mfano wa Mungu, inamaanisha taswira au mwonekano wa kimaumbile. Mungu ana maumbile kama yetu; yaani ana kichwa, mikono, miguu, kiuno, macho, kinywa, nywele na kadhalika kama nasi tulivyo na viungo hivi *{soma Danieli 7:9,13; Ufunuo 1:13-16}*. Lakini biblia inapozungumzia sura ya Mungu, inamaanisha akili na tabia ya Mungu ambayo hatukuumbwa kwayo *{soma 1 Wakorintho 15:49}*. Katika *Mwanzo 1:26* tumeona Mungu akikusudia kuumba mtu kwa mfano na sura yake, lakini baadaye tunaona kwamba mtu huyo aliumbwa kwa mfano pekee wa Mungu na wala si kwa sura yake; je, ni kwa nini ilikuwa hivyo?

Mungu alimuumba Mwanadamu katika hatua ya kwanza ambayo ni ya mwili wa damu na nyama. Na kabla ya kuanza hatua ya pili ya uumbaji ambayo ni kupewa na kujenga ufahamu *{yaani akili na tabia}* ambayo ndiyo kufanywa kwa sura ya Mungu; Mwanadamu alidanganywa na Shetani *{yule nyoka wa zamani}*, na hivyo badala ya kupokea akili ya Mungu, akapokea akili ya Shetani

{soma Mwanzo 2:15-17; 3:1-19}. Na hivyo Mungu akasitisha uumbaji wa Mwanadamu. Kwa sababu hiyo, Mwanadamu akakwamia katika hatua hiyo ya kwanza hadi leo.

Sasa basi; ikiwa mambo yako hivi; je, ni kusema kwamba, mpango wa Mungu wa kuitawala tena dunia kupitia kwa Mwanadamu umeshindwa kufikia malengo? La hasha! Mungu anasema, **“nitatenda kazi, naye ni nani awezaye kuizuia?” Isaya 43:13.** Kwa hakika hakuna, maana anaendelea kusema, **“nimenena, nami nitatekeleza; nimekusudia, nami nitafanya” Isaya 46:11.** Sasa basi; ikiwa Mungu hashindwi; ni nini anachofanya hivi sasa kuhusu mpango wake huo?

Sura ya tatu

WOKOVU

Kama tulivyoona ya kuwa, wakati Mungu alipokuwa akimuumba mtu, tayari Shetani alikuwa ndiye mtawala wa dunia hii na dhambi ilikuwamo ulimwenguni; na maisha ya Shetani huyo yanafananishwa na mti wa ujuzi wa mema na mabaya *{soma Mwanzo 2:9,17}; na kwa maelezo zaidi kuhusu hili, agiza ujumbe wetu usemao, “MITI MIWILP”, utakusaidia kulielewa jambo hili; kumbuka ujumbe huo utatumiwa bure kabisa}*. Kwa hivyo; Mungu alifahamu kwamba yawezekana mtu huyo akadanganywa. Na hivyo Mungu akaweka tayari mpango wa kumwokoia endapo itatokea kwamba mtu huyo atadanganyika. Na njia ya wokovu huo ilikuwa ni kusulibiwa kwa Yesu Kristo ambaye kwa mujibu wa mpango huo **“alichinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia” Ufunuo 13:8; soma pia Zaburi 40:6-7.** Jambo hili lina maana gani hasa? Twende pamoja tafadhali.

Tumeona jinsi ambavyo mwanadamu alidanganywa na Shetani na akadanganyika na kuyafuata maisha yake ambayo ni ya uharibifu na uovu na yaliyojawa na kila namna ya ubaya na taabu, tena yaliyo mafupi sana *{soma Mwanzo 3:1-19; Waefeso 2:1-3; Ayubu 14:1-2}*. Lakini pia tukaona ya kuwa, tayari Mungu alikuwa amekusudia kumwokoia kutoka katika maisha hayo ya uharibifu *{soma Ufunuo 13:8}*. Na hivyo basi; Mungu akaweka awamu *{vipindi}* tatu za wokovu wa wanadamu katika kuyafikia malengo yake ya kuitawala tena dunia kupitia kwa mwanadamu. **{DOKEZO; Mpendwa msomaji, tafadhali kuwa makini sana, maana haya unayojifunza hapa hivi sasa ni mafundisho ya kweli ya Mungu kupitia Biblia Takatifu; kwa hivyo ni siri za ufalme wa mbinguni na wala si mafundisho ya madhehebu ya kidini kama ilivyozoeleka; soma Mathayo 13:10-11; hivyo basi uwe na Biblia yako mkononi na ufuatane nasi katika kila kipengele ili kujua Biblia inasema nini, na Mungu ana mpango gani na wewe; asante}**.

Awamu ya kwanza ya wokovu

Tumeona dhamira ya Mungu ya kuitawala tena dunia kupitia kwa mwanadamu ikibaki pale pale akisema, **“nitatenda kazi, naye ni nani awezaye kuizuia?...nimenena, nami nitatekeleza; nimekusudia, nami nitafanya” Isaya 43:13; 46:11.** Lakini vile vile pia kwamba, ili mwanadamu aweze kuitawala dunia, ni lazima aumbike na kuwa kama Mungu mwenyewe; yaani aumbike kwa mfano *{kwa maumbile}* na kwa sura *{kwa tabia}* ya Mungu *{soma Mwanzo 1:26; 1 Wakorintho 15:15; Yohana 4:24; 3:5-6}*. Kutokana na hayo basi; Mungu aliwachagua wanadamu wachache waliokuwa tayari kuisikiliza sauti yake na akawafundisha njia yake; yaani sheria zake za haki ambazo ni maelezo ya maisha yake makamilifu na ambayo ndiyo sura *{tabia}* ya Mungu. Kwa maana nyingine ni kwamba; kwa wale walioisikia sauti yake, Mungu alianza hatua ya pili ya uumbaji ndani yao ambayo ni kupewa na kukuza akili *{yaani ufahamu wa Mungu, au tabia}* ya Mungu ambayo ni sura yake *{kwa maelezo zaidi kuhusu hili, agiza ujumbe wetu usemao, “JE, WEWE NI MKRISTO?”}*, na utatumiwa bure ili ujifunze zaidi).

Watu hao ni pamoja na Habili, Henoko, Nuhu, Ayubu, Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Yusufu, Musa, na wengine ambao walipokea ufahamu wa Mungu ndani yao kwa njia ya Roho Mtakatifu wa Mungu na wakaumbwa katika hatua ya pili ambayo ni kufahamu na kushika sheria za Mungu, yaani wakaumbika kwa sura {*kwa tabia*} ya Mungu. Kwa kuwa watu hao walimkataa Shetani na maisha yake; basi walipata upinzani mkali sana kutoka kwa huyo Shetani na majeshi yake ambao ndio watawala wa dunia kwa sasa na huku wakiwashinikiza watu wote duniani kuifuata njia yao {*soma Ufunuo 12:9*}. Lakini watu hao kwa kuipokea akili {*sura*} ya Mungu na kuyapenda maisha ya Mungu ya haki, basi kwa imani yao “*walishinda milki za wafalme, walitenda haki, walipata ahadi, walifunga vinywa vya simba, walizima nguvu za moto, waliokoka na makali ya upanga, Walitiwa nguvu baada ya kuwa dhaifu, walikuwa hodari katika vita, walikimbiza majeshi ya wageni*” *Waebrania 11:33-34*. Na hatimaye, watu hao “*wakafa katika imani, wasijazipokea zile ahadi* {yaani ahadi ya uzima wa milele pamoja nakuitawala dunia}, *bali wakazona tokea mbali na kuzishangilia, na kukiri kwamba walikuwa wageni na wasafiri juu ya nchi*” *Waebrania 11:13*.

Ni kwa nini watu hao hawakuipokea ahadi ya kuitawala dunia pamoja na uzima wa milele, na badala yake wakafa katika imani ya kuzipokea ahadi hizo baadaye? Ni kwa sababu, walikuwa sasa wamekamilika katika hatua mbili tu za uumbwaji wao, na bado hawajaifikia hatua ya tatu na ya mwisho ya uumbwaji ambayo ni kubadilishwa na kufanywa kuwa viumbe wa kiroho {*soma 1 Wakorintho 15:50*}. Na kwa habari ya kufikia hatua ya tatu ya uumbwaji ambayo ni ya ukamilifu, biblia inasema, “*Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi; kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi*” *Waebrania 11:39-40; soma pia 1 Wathesalonike 4:16-17*. Watu hao ni wa kwanza kuchaguliwa {*ama kuitwa*} katika awamu ya kwanza ya wokovu wa ulimwengu, lakini si wao peke yao wanaokamilisha kundi hilo la awamu ya kwanza. Tafadhali twende pamoja.

Ujio wa Kristo mara ya kwanza

Kwa muda mrefu Mungu “*aliwaacha mataifa yote waende katika njia zao wenyewe* {*Matendo 14:16*}; {*isipokuwa baadhi ya watu wachache tu ambao tumeona habari zao hapo juu wakitembea katika njia sahihi ya Mungu*} wakifuata mawazo yao wenyewe, na kutenda kila mmoja kwa kufuata ushupavu wa moyo wake mbaya ambayo ni roho ya uovu waliyoipokea kutoka kwa Shetani {*soma Yeremia 18:12*}

Lakini baadaye, “*hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe* {yaani Yesu Kristo} *ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria, kusudi awakomboa hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana*” *Wagalatia 4:4-5* {*kumbuka mpango huu wa wokovu ulikusudiwa tangu mwanzo kama tulivyoona hapo awali; soma Ufunuo 13:8*}. Hapa tunaona kwamba, Mungu amemtuma Yesu Kristo kuwafundisha wanadamu maisha ya haki na ya kweli ambayo walidanganywa na wakayapuuzwa tangu pale Edeni {*soma Mwanzo 3:4-6*}.

Wakati Yesu Kristo alipokuja, aliwaletea Wanadamu ujumbe aliopewa na Mungu. Na ujumbe huo aliouleta Yesu kwa wanadamu kutoka kwa Mungu ulihusu ujio wa ufalme wa Mungu ambao utaitawala dunia yote. Ulikuwa pia ni wito kwa wanadamu kwamba wageuze njia zao za maisha na wajifunze njia ya maisha ya Mungu ili waweze kurithi na kutawala katika ufalme huo.

Na hapa Yesu anasema, “*Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini injili*” *Marko 1:15*. Naam; ufalme ule ambao Mungu anataka kuurejesha uko karibu. Lakini kuna kikwazo mbele yetu. Mfumo wa maisha haya tuliyorithi kutoka kwa Adamu hauwezi kuutawala ufalme ule. Ni lazima tugeuke {*tutubu*} kutoka katika mfumo {*au mtindo*} huu wa maisha kabla ya kuuingia ufalme huo. Tugeukie wapi? {*Kwa maelezo zaidi kuhusu hili, agiza ujumbe wetu usemao, “WAPI PAKUANZIA”, kwa msaada zaidi na utatumiwa bure*}.

Toba na msamaha

Kama ilivyokuwa kwa akina Ibrahimu na wengineo tulioona habari zao hapo awali{soma *Mwanzo 12:1-4*}; ndivyo Mungu anavyoendelea kuwaita watu kupitia kwa Yesu Kristo ili watoke katika utumwa wa dhambi na mauti, waingie katika utumwa wa haki na uzima {soma *Warumi 6:16-18*}. Na kwa habari ya wito huo, si maamuzi {au matakwa} ya mtu awaye yote kwa fikira na akili zake mwenyewe kuamua kumgeukia Mungu, bali ni Mungu mwenyewe kwa mapenzi na matakwa yake anawachagua na kuwaita wale aliowakusudia wamgeukie na kumwendea. Yesu anasema; **“Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba...”** *Yohana 6:44*. Kwa hali hiyo basi; hata leo hii, wito huu unazidi kutolewa kwa wanadamu, lakini si wote wanaousikia wanauelewa na kuuitikia kama ilivyoandikwa; **“Na neno la nabii Isaya linatimia kwao, likisema, Kusikia mtasikia, wala hamtaelewa; Kutazama mtatazama, wala hamtaona. Maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, Na kwa masikio yao hawasikii vema, Na macho yao wameyafumba; Wasije wakaona kwa macho yao, Wakasikia kwa masikio yao, Wakaelewa kwa mioyo yao, Wakaongoka, nikawaponya”** *Mathayo 13:14-15*. Naam; hii ni kwa sababu watu hao wakati wa kuokolewa kwao haujawadia, si wa awamu hii ya kwanza ya wokovu.

Lakini hebu na tuwazungumzie wale waliokusudiwa wokovu katika awamu hii ya kwanza. Wao Mungu huwajalia kusikia na kuelewa na kisha kumfuata Kristo na kujifunza kwake zaidi kama Yesu anavyosema kuwa, **“Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata”** *Yohana 10:27*. Na tena; **“...heri macho yenu, kwa kuwa yanaona; na masikio yenu, kwa kuwa yanasikia”** *Mathayo 13:16*. Watu hawa wakiisha kuupokea wito wa Mungu na kumwendea, hatimaye hupewa **“uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu”** soma *Yohana 1:12* {kwa maelezo zaidi kuhusu ni jinsi gani Mungu anawafanya kuwa watoto wake; basi agiza ujumbe wetu usemao **“JE, WEWE NI MKRISTO?”, na utatumiwa bure**}. Kwa hivyo wapendwa; ikiwa unasikia wito wa Mungu ndani ya moyo wako hivi sasa, basi ushauri ni huu kwamba, **“Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina kale Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie”** *Matendo 2:38-39*.

Kundi hili la walioitwa na Mungu kwa kuyatimiza makusudi yake ndilo **“KANISA LA MUNGU”** ambalo Yesu Kristo mwenyewe alilijenga {soma *Mathayo 16:18; Matendo 2:47; 9:31; 12:5; 1 Wakorintho 11:22; Waefeso 2:19-22; 1 Wathesalonike 2:14; na 1 Timotheo 3:5*}. Hawa ndio ambao Yesu anawaambia, **“Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme”** *Luka 12:32*.

Ni kwa nini Mungu amelichagua kundi hili dogo na kukusudia kulipatia ule ufalme wake ujao? Ni nini madhumuni hasa ya kuliweka kundi {au Kanisa} hili? Kama tulivyoona hapa awali kwamba, mpango wa Mungu ni kuurejesha tena ufalme wake katika dunia hii na kuuondosha kabisa huu ufalme wa sasa wa Shetani unaoitawala dunia kwa sasa. Bado Mungu anaendelea na mpango wake huo kwa namna ya pekee sana. Ni hivi punde tu, Mungu atausimamisha ufalme wake katika dunia hii. Na ufalme huo utatawaliwa na kundi {Kanisa} hili dogo alilolichagua Mungu. Lakini kabla hawajakabidhiwa ufalme huo, hivi sasa Mungu analiimarisha kundi hili katika kanuni za ufalme huo wa mbinguni; naam, hivi sasa anawafundisha amri, sheria, shuhuda na hukumu za haki ambazo kwazo watazitemia kuitawala dunia yote. Na kanuni pamoja na sera za ufalme huo wa mbinguni ni kuishi kwa kufuata {kwa kushika} amri za Mungu na kuwa na imani ya Yesu Kristo {soma *Ufunuo 14:12; 12:17; Mathayo 19:17*}. Naam; Mungu anawaumba katika hatua ya pili ambayo ni kupewa na kukuza akili na tabia ya Mungu ndani yao, ambayo ni kuumbwa kwa sura ya Mungu. {Na kwa maelezo zaidi kuhusu kanuni hizo za ufalme wa Mungu, agiza kitabu chetu kisemacho, **“AMRI KUMI ZA MUNGU”**, pamoja na ujumbe usemao, **“JE, WEWE NI MKRISTO?”**, utatumiwa bure ili ujifunze zaidi}.

Naam; Kanisa hili ambalo ni kundi dogo, linaandaliwa kuwa **WAFALME**{yaani, watawala}**NA MAKUHANI**{yaani, waalimu wa neno la Mungu}**WA MUNGU** katika ule ufalme ujao {soma *Kutoka 19:5-6; 1 Petro 2:9; Ufunuo 5:10*}.

Sura ya nne

UJIO WA KRISTO MARA YA PILI

Vita vya mwisho

Ujio wa Kristo mara ya pili hapa duniani tunaoutarajia hivi punde utatanguliwa na vita kubwa sana ya ulimwengu wote na ambayo itakuwa ndiyo vita ya mwisho kushuhudiwa katika dunia. Mataifa makubwa yenye nguvu ya dunia yatakuwa yamegawanyika pande mbili na kupigana vita ambayo kama Mungu hataingilia kati, basi wanadamu watajimaliza wenyewe na kuangamiza uhai wote juu ya dunia kutokana na silaha hatari zilizopo na zinazoendelea kuboreshwa hivi sasa kama Nyuklia {*Nuclear*}, Atomiki {*Atomic*} na nyinginezo zenye sumu hatari. Katika kipindi hicho ndipo atakapotokea Yesu Kristo na kuinusuru dunia na maangamizi makubwa yanayoikabili. Nabii Zakaria anasimulia jinsi mambo yatakavyokuwa wakati huo kabla ya ujio wa Kristo pamoja na kuja kwake pia; na hapa anasema; ***“Tazama, siku moja ya BWANA inakuja, ambayo mateka yatagawanyika kati yako. Kwa maana nitawakusanya mataifa yote walete vita juu ya Yerusalemu; na huo mji utapigwa, nazo nyumba zitatekwa, nao wanawake watatendwa jeuri; na nusu ya watu wa mji watatoka kwenda utumwani; ila mabaki ya watu wa mji hawatakatiliwa mbali. Hapo ndipo atakapotokea BWANA, naye atapigana na mataifa hayo, kama vile alipopigana zamani siku ya vita”*** Zakaria 14:1-3. Soma pia *Ufunuo 16:12-16*.

Ni kwa nini BWANA {yaani, Yesu Kristo} atapigana na mataifa hayo ambayo yalikuwa yakipigana yenyewe? Wakati mataifa hayo yatakapokuwa yakipigana; ghafla Yesu Kristo atatokea hewani kwa kishindo kikubwa sana akiwa na majeshi ya mbinguni. Kutokana na tukio hilo, haraka sana Shetani atayashawishi majeshi hayo ya ulimwengu ili waache kushambuliana wenyewe, na badala yake, wataungana na kuanza kupigana vita na huyo Kristo ajaye na majeshi yake. Nabii Yohana anasema, Shetani atawapa ***“shauri moja, nao wampa yule mnyama nguvu zao na mamlaka yao. Hawa watafanya vita na Mwana-kondoo {yaani na Yesu Kristo}, na Mwana-kondoo atawashinda, kwa maana Yeye ni Bwana wa Mabwana, na Mfalme wa Wafalme,...”***Ufunuo 17:13-14. Soma pia *Mathayo 24:30; Zakaria 14:12-13*. {Kwa maelezo ya kina zaidi kuhusu vita hivi, agiza ujumbe wetu usemao, ***“VITA VYA HAR-MAGEDONI”***, na utatumiwa bure}.

Ufufuo wa kwanza

Ujio huo wa Kristo kwa nguvu na utukufu mwingi {soma *Mathayo 24:29-30; Luka 21:25-27*}, utaambatana pia na ufufuo wa kwanza. Ufufuo huu wa kwanza utawapata wale tu waliokufa katika Kristo Yesu, yaani Watakatifu wote walioitwa katika awamu ya kwanza ya wokovu na wakafa kabla ya ujio wa Kristo; naam, hao peke yao ndio watakaofufuka wakati huo. Mtume Paulo anafafanua jambo hili akisema; ***“Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza” 1 Wathesalonike 4:16.***

Kwa habari ya ufufuo huu wa kwanza, nabii Yohana anaandika akisema, ***“...nao {watakatifu} wakawa hai, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu. Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu. Huo ndio ufufuo wa kwanza. Heri, na mtakatifu, ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya hao mauti ya pili {yaani ziwa la moto} haina nguvu; bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu” Ufunuo 20:4-6.***

Watakatifu hao wakiisha kufufuliwa, wataungana na wale watakatifu watakaokuwa hai wakati huo, na kwa dakika moja watabadilishwa na kuwa viumbe wa kiroho. Mtume Paulo anafafanua tena akisema; ***“Angalieni, nawaambia ninyi siri; hatutalala {hatutakufa} sote, lakini sote tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika. Maana sharti huu {mwili} uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa” 1 Wakorintho 15:51-53.***

Na kufikia hapo, Watakatifu hao watakuwa wamekamiliwa katika uumbwaji wao. Kumbuka tuliona kwamba mwanadamu sharti apitie hatua kuu tatu katika kuumbwa kwake na ndipo awe ameumbwa kwa mfano na sura ya Mungu na kuwa kama Mungu ndipo aweze kuitawala dunia kulingana na mpango wa Mungu ulivyo {soma *Mwanzo 1:26; 1 Wakorintho 15:50,53; Waebrania 11:39-40*}. Baada ya watu hao kubadilishwa na kuwa viumbe wa kiroho kama Mungu alivyo {soma *Yohana 4:24; 3:5-6*}, watakuwa na uwezo wa kuruka {kupaa} hewani kama malaika. Na hapa tena Paulo anaelezea akisema; ***“Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele” 1 Wathesalonike 4:17.***

Kutoka hapo hewani {mawinguni}, Kristo, majeshi ya mbinguni pamoja na hao watakatifu waliompokea watateremka chini hadi kutua juu ya mlima wa Mizeituni. Nabii Zakaria anaelezea akisema; ***“Na siku hiyo miguu yake itasimama juu ya mlima wa Mizeituni, unaoelekea Yerusalemu upande wa mashariki, nao mlima wa Mizeituni utapasuka katikati yake, upande wa mashariki na upande wa magharibi...” Zakaria 14:4.*** Naam; Yesu Kristo na jeshi lake lote watateremka na kutua juu ya mlima wa Mizeituni. Ni mlima ule ule ambao wakati wa kupaa kwake kwenda mbinguni baada ya kufufuka kwake, Yesu huyo alichukuliwa kutoka juu yake na mawingu. Luka anatukumbusha tukio hilo akisema; ***“{Yesu}Akiisha kusema hayo, walipokuwa wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao. Walipokuwa wakikaza macho mbinguni, yeye alipokuwa akienda zake, tazama, watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe, wakasema, Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni”***

“Kisha {wanafunzi} wakarudi kwenda Yerusalemu kutoka mlima ulioitwa wa Mizeituni, ulio karibu na Yerusalemu...” Matendo 1:9-12.

Ufalme wa mbinguni warejeshwa duniani

Ni kuanzia hapo Yerusalemu ndipo ambapo huyo Kristo aliyeteremka kutoka mbinguni akiwa na majeshi yake atakapokiweka kiti chake cha enzi na kuanza kuitawala dunia yote. Mji huo wa Yerusalemu ndio utakaokuwa Makao Makuu ya utawala wa Kristo {yaani makao makuu ya ufalme wa mbinguni} hapa duniani. Nabii Yeremia anatuambia kwamba; **“Wakati ule watauita Yerusalemu kiti cha enzi cha BWANA; na mataifa yote watakusanyika huko Yerusalemu, kwa ajili ya jina la BWANA; wala hawatakwenda tena kwa ukaidi wa moyo wao mbaya”** Yeremia 3:17.

Baada ya Kristo kuketi juu ya kiti chake cha enzi kama Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana {soma Ufunuo 17:14}; ndipo atakapoweka muundo mpya wa uongozi na utawala wa dunia yote. Viongozi na watawala watakaowekwa na Kristo si wengine bali ni wale Watakatifu wake waliobadilishwa na kuwa viumbe wa kiroho na kufikia hatua ya ukamilifu kama Kristo mwenyewe alivyo {soma Waefeso 4:13}. Nabii Danieli analithibitisha jambo hili akisema; **“Na katika siku za wafalme hao {wakati atakapokuja Kristo} Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi {za dunia}zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele”** Danieli 2:44. Tena Danieli anasema; **“Na ufalme, na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote {yaani duniani kote}, watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu; ufalme wake ni ufalme wa milele, na wote wenye mamlaka {yaani watawala watakaokuwako wakati huo wa ujio wa Kristo} watamtumikia na kumtii”** Danieli 7:27.

Naam; iko wazi kabisa kuwa Watakatifu watapewa kuitawala dunia yote chini ya Mfalme Mkuu Yesu Kristo. Yesu huyo aliahidi kupitia kwa nabii Yohana akisema; **“Na yeye ashindaye, na kuyatunza matendo yangu hata mwisho, nitampa mamlaka juu ya mataifa, naye atawachunga kwa fimbo ya chuma...”**. Na tena; **“Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi...”** Ufunuo 2:26-27; 3:21; soma pia Luka 19:15-19.

Wafalme na Makuhani wa Mungu

Punde tu kabla ya Kristo kuusimamisha ufalme wake hapa duniani, Shetani atanyang’anywa mamlaka yake na kuwekwa kifungoni. Yohana anaelezea katika kitabu cha ufunuo akisema; **“Kisha nikaona malaika akishuka kutoka mbinguni, mwenye ufunguo wa kuzimu, na mnyororo mkubwa mkononi mwake. Akamshika yule joka, yule nyoka wa zamani, ambaye ni Ibilisi na Shetani, akamfunga miaka elfu; akamtupa katika kuzimu, akamfunga, akatia muhuri juu yake, asipate kuwadanganya mataifa tena, hata ile miaka elfu itimie; na baada ya hayo yapasa afunguliwe muda mchache”** Ufunuo 20:1-3. Naam; Shetani atawekwa kifungoni ili **“asipate kuwadanganya mataifa tena”**. Jambo hili litafanyika ili wanadamu wa mataifa yote wapate nafasi bila kikwazo ya kujifunza njia ya Mungu ya uzima kupitia kwa wale Watakatifu wa Mungu ambao ni Kanisa lake teule. {Kwa maelezo zaidi kuhusu kifungo cha Shetani miaka elfu moja; agiza kitabu chetu kisemacho, **“SIKUKUU ZA MUNGU”**, ili ujifunze zaidi, na utatumiwa kitabu hicho bure}.

Japokuwa Watakatifu hao Mungu atawafanya kuwa Wafalme pamoja na Kristo; lakini pia atawafanya kuwa Makuhani {yaani Waalimu wa neno la Mungu} wake ili waufundishe ulimwengu wote sheria za Mungu za haki. Huu hapa ushahidi wa maandiko; **“Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki {utawala} ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu”** 1 Petro 2:9. Na tena; **“ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki {wanatawala} juu ya nchi {duniani}”** Ufunuo 5:10; soma pia Kutoka 19:5-6.

Kama tulivyoona ya kuwa Makao Makuu ya ufalme wa mbinguni juu ya dunia yatakuwa pale Yerusalemu; basi mambo yote ya kitawala na kielimu {ama kidini} yatatokea hapo. Na kwa

sababu hiyo basi; ***“mataifa mengi watakwenda na kusema, Njoni, twende juu mlimani kwa BWANA, nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake maana katika Sayuni itatoka sheria, na neno la BWANA katika Yerusalemu” Isaya 2:3; soma pia Mika 4:2.***

Naam; Watakatifu watasaidiana na Yesu Kristo katika huu mpango wa elimu ya Mungu kwa wote, kuwasaidia wengine kuzijua njia za Mungu. Akiuzungumzia wakati huo, nabii Isaya alisema waalimu ***“hawatafichwa tena, ila macho yako yatawaona waalimu wako; na masikio yako yatasikia neno nyuma yako, likisema, Njia ni hii, ifuateni, mgeukapo kwenda mkono wa kulia, na mgeukapo kwenda mkono wa kushoto” Isaya 30:20-21.*** Nafasi ya kuwasaidia wengine kumfahamu na kupatanishwa na Mungu ni wito wa pekee sana. Kila atumikaye katika huduma hiyo ataitwa ***“Mwenye kutengeneza mahali palipobomoka; na, Mwenye kurejeza njia za kukalia” Isaya 58:12.*** Tena wataitwa ***“Waokozi” {soma Obadia 1:21}.***

Mungu anawaita watu kutoka katika ulimwengu kwa wakati huu wa sasa ili wawe wateule wake, waliotakaswa na kukombolewa naye ***{soma 2 Wakorintho 6:16-7:1}.*** Tena, ili waishi maisha mfano wa yale ambayo Mungu anawatayarisha kuhudumu kwayo katika kipindi cha Milenia *{miaka elfu moja}* cha utawala wa Yesu. Kutokana na utekelezwaji wa mpango huo wa elimu ya Mungu kwa ulimwengu wote, basi ***“dunia itajawa na kumjua BWANA, kama vile maji yanavyoifunika bahari” Isaya 11:9; soma pia Habakuki 2:14.***

Katika kipindi hicho, watu wa dunia yote watazungumza lugha moja, tena iliyo safi kama Mungu alivyoahidi kwa kinywa cha nabii Sefania akisema; ***“Maana hapo ndipo nitakapowarudishia mataifa lugha iliyo safi, wapate kuliitia jina la BWANA, wamtumikie kwa nia moja” Sefania 3:9.***

Ulimwengu wa Amani tele

Katika kipindi hicho, Kristo atawaleta viumbe wote katika mahusiano kamili na Mungu, na amani mara itarejeshwa. Mfalme Daudi anasema; ***“Wana amani nyingi waipendao sheria yako...” Zaburi 119:165.*** Hebu fikiria jinsi ulimwengu utakavyokuwa, pindi ambapo kila mmoja atazifahamu sheria za Mungu na kuishi kwazo!

Awali ya yote, ufahamu zaidi unahitajika kwanza ili kujua kuhusu mabadiliko haya ya pekee. Mabadiliko ya kiroho yatafanyika katika watu. Mungu anaongea kupitia kwa nabii Ezekieli, akieleza jinsi ambavyo jambo hili litafanyika; ***“Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama. Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda” Ezekieli 36:26-27.*** Roho wa Mungu atawawezesha watu kunuwia na kutaka kwa dhati kumtii Mungu kutoka mioyoni mwao. Wataanza kuwafikiria *{ama kuwaona}* wengine kuwa ni ***“bora kuliko nafsi zao” {Wafilipi 2:3}.*** Badala ya ubinafsi unaowatawala watu kwa sasa, malengo yao yatakuwa katika kuwasaidia wenzao. Wizi hautakuwapo tena! Hakutakuwa na ulinzi wa mali; kwa sababu ulimwengu utakuwa katika amani, na mataifa ***“watafua panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe miundu; taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine, wala hawatajifunza vita tena kamwe” Isaya 2:4; tazama pia Mika 4:3.***

Katika kipindi hiki cha miaka elfu moja, Mungu ataibadili hata asili ya wanyama iendane na amani itakayokuwa katika jamii. Akiuzungumzia wakati huo, nabii Isaya anasema; ***“Mbwa-mwitu atakaa pamoja na mwana-kondoo, na chui atalala pamoja na mwana-mbuzi; ndama na mwana-simba na kinono watakuwa pamoja, na mtoto mdogo atawaongoza. Ng’ombe na dubu watalisha pamoja; watoto wao watalala pamoja; na simba atakula majani kama ng’ombe. Na mtoto anyonyaye atacheza penye tundu la nyoka, na mtoto aliyeachishwa atatia mkono wake katika pango la fira. Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima {ama ufalme} wangu wote mtakatifu...” Isaya 11:6-9.***

Kuponywa madhara ya dhambi

Mungu ataponya magonjwa {*maradhi*} na madhaifu yote ya kimwili. Isaya alitabiri kuhusu wakati huo ambao *“macho ya vipofu yatafumbuliwa, na masikio ya viziwi yatazibuliwa. Ndipo mtu aliye kilema atarukaruka kama kulungu, na ulimi wake aliye bubu utaimba...”* Isaya 35:5-6. Hata hivyo umuhimu mkubwa wa uponyaji utakuwa ni kuhusu uponywaji wa kiroho. Isaya alitabiri kuwa Yesu Kristo atakamilisha uponyaji aliouanza tangu kipindi cha utume wake duniani; *“Roho ya Bwana MUNGU Ijuu yangu; kwa sababu BWANA amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema; amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao. Kutangaza mwaka wa BWANA uliokubaliwa, na siku ya kisasi cha Mungu wetu; kuwafariji wote waliao; kuwaagizia hao waliao katika Sayuni, wapewe taji ya maua badala ya majivu, mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito;...”* Isaya 61:1-3; tazama pia Luka 4:18-19. Madhara yote yapatikanayo katika vizazi vyote vya wanadamu ambayo chanzo chake ni kufuata njia ya Shetani ya dhambi yataponywa.

Kupitia kwa Isaya, Mungu alizungumzia jinsi jangwa litakavyoponywa na kuwa nchi {*ardhi*} izaayo, *“maana katika nyika maji yatabubujika; na vijito jangwani. Na mchanga ung’aa mfano wa maji utakuwa ziwa la maji”* Isaya 35:6-7. Katika kipindi hicho nchi itazaa mavuno tele. *“Angalieni, siku zinakuja, asema BWANA, ambazo huyo alimaye atamfikilia avunaye, na yeye akanyagaye zabibu atamfikilia apandaye mbegu; nayo milima itadondoza divai tamu, na vilima vyote vitayeyuka”* Amosi 9:13.

Kufunguliwa kwa Shetani

Na baada ya mambo hayo yote kutimia kama yasemavyo maandiko matakatifu ya Mungu; yaani baada ya hiyo miaka elfu moja kutimia; ndipo Shetani atakapofunguliwa atoke kifungoni mwake ili apate kuwajaribu watu hao waliofundishwa sheria za Mungu na pia kushuhudia utawala wa amani wa ufalme wa mbinguni. Lakini jambo hilo litachukua muda mfupi sana. Biblia inasema, *“...hata ile miaka elfu itimie; na baada ya hayo yapasa afunguliwe muda mchache”* Ufunuo 20:3. Ifahamike kwamba, Mungu kamwe hatamlazimisha mtu awaye yote kuchagua kuishi maisha ya uzima wa milele; bali akiisha kumuonesha mtu yaliyo mema na yaliyo mabaya, Yeye Mungu humwacha mtu huyo achague mwenyewe lile atakaloambatana nalo, japo pia Mungu hutushauri kuchagua na kuambatana na yaliyo mema {*soma Torati 11:26-28; Isaya 48:17-18; Marko 16:16*}; tena hii ikiwa ni kwa faida yetu sisi wenyewe.

Hivyo basi, ni wazi kwamba watu wengi sana kwa vile watakuwa wameonja ladha halisi ya ufalme wa mbinguni; yaani huo utawala bora ajabu wa Yesu Kristo na Watakatifu wake; watampinga Shetani vilivyo {*wataukataa udanganyifu wa Shetani*} ili waendeleo kuambatana na Mungu wao katika hayo maisha ya amani na raha mustarehe kabisa.

Lakini vile vile wapo watu wengine wengi pia ambao watakaidi na kufuatana na huyo Shetani katika udanganyifu wake. Biblia inasema; *“Na hiyo miaka elfu itakapokwisha, Shetani atafunguliwa, atoke kifungoni mwake; naye atatoka kuwadanganya mataifa walio katika pembe nne za nchi, Gogu na Magogu, kuwakusanya kwa vita, ambao hesabu yao ni kama mchanga wa bahari”* Ufunuo 20:7-8. Inashangaza kuona kwamba kuna watu wengine wengi sana, gogu na magogu, tena wengi kama mchanga wa bahari wasiopenda maisha ya amani na utulivu; bali wapendao maisha bandia yaliyojaa kila namna ya mateso, vurugu na uchafu wote. Hata hivyo; muanzilishi wa maisha, yaani Mungu; hatakubaliana na watu hao kamwe, kwani hayo siyo makusudi

yake ya kuyaanzisha maisha. Lakini lengo hapa hasa la Mungu ni kwamba, kila mtu ashuhudiwe habari njema ya uzima wa milele na aijue kweli yote kumuhusu Mungu, maisha yake na makusudi yake ya uumbaji wa mwanadamu; ili atakayependezwa na mpango wake huo, aambatane naye; na wale wasiokubaliana na mpango huo, basi na waambatane na Shetani, na hivyo asiwepo ye yote atakayetoa hudhuru kwamba hakujulishwa matakwa {mapenzi/makusudi} ya Mungu. Na hii ndiyo awamu ya pili ya wokovu ama ukombozi wa wanadamu kutoka katika utumwa mbaya wa dhambi na mauti ili kuingia katika uhuru wa haki na uzima wa milele pamoja na Mungu mwenyewe.

Lakini je, hao watakaoendelea kumuasi Mungu na kuambatana na Shetani, ni nini hatima yao? Baada ya kuwa Shetani amewakusanya watu hao, atawashawishi ili wapigane vita na Watakatifu na kwamba waupindue ufalme wa Kristo. Biblia inasema; **“Wakapanda juu ya upana wa nchi, wakaizingira kambi ya watakatifu, na mji huo uliependwa {yaani Yerusalemu ambao utakuwa ni Makao Makuu ya utawala wa Kristo}. Moto ukashuka kutoka mbinguni, ukawala {ama ukawateketeza}. Na yule Ibilisi, mwenye kuwadanganya, akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti, alimo yule mnyama na yule nabii wa uongo...” Ufunuo 20:9-10.**

Baada ya Shetani na jeshi lake kuteketezwa kwa moto; ni kitu gani kitafuata? Habari gani juu ya mamilioni ya watu wa vizazi vilivyopita walioishi na kufa bila ufahamu wala kuisikia kweli ya Mungu? Na vipi kuhusu wale watakaokufa katika vita vya ujio wa Kristo? Ni kwa namna gani Mungu atawapa wokovu? Sura ifuatayo inatoa majibu.

Sura ya tano

AWAMU YA TATU YA WOKOVU

Uzima wa milele kutolewa kwa wote

Biblia inaeleza wazi katika kitabu cha **Matendo 4:12** kwamba, **“hapana jina jingine chini ya mbingu”** zaidi ya hili jina la Yesu Kristo ambalo wanadamu wanapaswa kuokolewa kwalo. Kipengele hiki kinaibua maswali mengi kwa ye yote anayeamini kwamba Mungu anajaribu kuuokoa ulimwengu mzima katika kipindi hiki. Ikiwa hiki ndicho kipindi pekee cha wokovu, ni lazima tukubaliane kwamba, huduma ya Yesu ya kuwaokoa wanadamu imeshindwa. Hii ni kwa sababu, mabilioni ya watu waliishi na kufa bila kusikia hata mara moja kuhusu jina la Yesu. Na mpaka sasa, maelfu ya watu wanakufa kila siku pasipo kusikia habari za Yesu. Hata pamoja na utume wa injili katika karne zote, bado ni wazi kwamba roho za wanadamu **“zidakazopotea”** ni nyingi sana zaidi ya zile **“zidakazookolewa”**. Ikiwa Mungu ni mwenye nguvu na uwezo, ni kwa nini basi wengi hawakuisikia injili ya wokovu? Ikiwa mambo yako hivi, basi vita baina ya Mungu na Shetani juu ya roho za wanadamu vinatoa mtazamo unaoashiria kwamba Mungu amelemewa.

Lakini hebu tujjulize, ni nini hatima ya watu hao? Je, Mungu ana mpango gani na wale wote ambao hawakusikia wala kufahamu lo lote kuhusu ukweli wa Mungu? Je, Muumbaji atawaweka wapi katika mpango wake? Je, watu hao wamepotea milele pasipo matumaini yo yote ya wokovu?

Hatuna sababu ya kutilia mashaka nguvu ya Mungu ya wokovu! Hebu sasa tupate ufumbuzi wa maswali yetu kutoka kwake na kufahamu ukweli wa neno lake.

Ufufuo wa pili kwa nafasi ya wokovu

Ili kupata majibu ya maswali yote hayo, ni lazima kutafakari swali ambalo wanafunzi walimuuliza Kristo punde tu kabla ya kuchukuliwa mbinguni wakisema; **“Je! Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme?” Matendo 1:6.** Wakati wanafunzi walipozungumzia matengenezo hayo, walifahamu kwamba ni kutokana na unabii mwingi uliotolewa juu ya taifa la

Israeli kuimarishwa tena. Moja kati ya unabii huo unapatikana katika *Ezekieli 37*. Sehemu hii inazungumzia maono ya nabii Ezekieli kuhusu bonde lililojaa mifupa mikavu. Na Mungu anamuuliza nabii Ezekieli akisema; **“Mwanadamu, je! mifupa hii yaweza kuishi?”** Naye nabii akajibu; **“Ee Bwana MUNGU, wajua wewe”**. Kisha Mungu anaiambia mifupa hiyo mikavu; **“Tazama, nitatia pumzi ndani yenu, nanyi mtaishi. Nami nitatia mishipa juu yenu, nami nitaleta nyama iwe juu yenu, na kuwafunika ngozi, na kutia pumzi ndani yenu, nanyi mtaishi; nanyi mtajua ya kuwa mimi ndimi BWANA”** *Ezekieli 37:5-6*.

Katika maono haya, ufufuo mwingine ambao ni wa pili unafanyika. Ufufuo huu wa pili ni wa kimwili; kwa maana kwamba, wote watakaofufuliwa watarudi kuwa hai wakiwa katika hali yao ya awali ya mwili wa damu na nyama. Mungu amesema atatia **“mishipa, nyama na ngozi”** juu ya watu hao na kutia **“pumzi {rejea Mwanzo 2:7}”** ndani yao, nao wataishi. Tafadhali elewa na fahamu tofauti iliyopo kati ya ufufuo huu wa pili na ufufuo ule wa kwanza. Ufufuo wa kwanza ni wa kiroho; kwa maana kwamba, wale watakaofufuliwa katika ufufuo huo, watafufuliwa na kubadilishwa moja kwa moja kuwa viumbe wa kiroho na si wa mwili huu wa damu na nyama uharibikao *{soma I Wakorintho 15:50-53; Ufunuo 20:6; Waebrania 11:35; ama rejea tena mada isemayo “Ufufuo wa kwanza”}*. Lakini ufufuo huu wa pili unawaleta watu katika maisha ya kawaida ya awali, yaani wenye miili iwezayo kufa na kuharibika.

Maandiko yanaeleza kuwa watu hawa walikuwa wamepoteza matumaini; **“Mifupa yetu imekauka, matumaini yetu yametupotea; tumekatiliwa mbali kabisa”** *Ezekieli 37:11*. Hata hivyo, Muumba wao anawatangazia matumaini ya ufufuo na kipawa cha Roho Mtakatifu katika kuwarejesha kuwa hai. Katika maono haya ya kipekee, Taifa la Israeli linatajwa kwa niaba ya watu wote ambao walikufa pasipo kupata nafasi ya wokovu, na Mungu atawafufua katika maisha ya kimwili. Mungu akasema; **“Tazama, nitafunua makaburi yenu, na kuwapandisha kutoka katika makaburi yenu, enyi watu wangu... Nami nitatia roho yangu ndani yenu, nanyi mtaishi”** *{mstari wa 12,14}*. Katika wakati huo ujao Mungu atatoa bure maji ya uzima ya kiroho ambayo ni Roho wake Mtakatifu.

Mungu **“atafanya agano la amani pamoja nao; litakuwa agano la milele pamoja nao;... Tena maskani yangu itakuwa pamoja nao; nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu”** *{mstari wa 26-27}*.

Mtume Paulo pia alilizungumzia hivi tukio hilo la wakati huo ujao; **“Basi. nauliza, Je! Mungu aliwasukumia mbali watu wake? Hasha! Kwa kuwa mimi nami ni Mwisraeli, mmoja wa wazao wa Ibrahimu, mtu wa kabila ya Benyamini. Mungu hakuwasukumia mbali watu wake aliwajua tokea awali”** *Warumi 11:1-2*. Na kama Paulo alivyoandika; **“Israeli wote wataokoka”** *{mstari wa 26}*; si Waisraeli tu, bali wote ambao hawakupata nafasi ya kunywa maji ya uzima ya neno la Mungu na Roho wake Mtakatifu watakuwa na nafasi hiyo *{soma Warumi 9:22-26}* Mungu atawapa bure nafasi ya uzima wa milele.

Kiti cha enzi kikubwa cheupe cha hukumu

Katika *Ufunuo 20:5* Yohana aliandika kwamba; **“Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu”**. Hapa Yohana ameweka wazi tofauti baina ya ufufuo wa kwanza, utakaofanyika katika ujio wa Kristo mara ya pili *{mstari wa 4,6}*, na ule ufufuo wa pili, utakaofanyika mwishoni mwa utawala wa miaka 1,000 ya Kristo. Kumbuka kwamba ufufuo wa kwanza ni wa uzima wa milele; tofauti na itakavyokuwa katika ufufuo wa pili, ambao Mungu atawafufua watu katika hali ya miili ya damu na nyama. Yohana akazungumzia pia huo ufufuo wa pili wa kimwili ambao Ezekieli aliandika habari zake; **“Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na yeye aliyeketi juu yake; ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana. Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima, na hao**

wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao. Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake; na Mauti na Kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake. Wakahukumiwa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake” Ufunuo 20:11-13.

Wafu waliosimama mbele ya Muumba wao ni wale wote ambao walikufa pasipo kumjua Mungu wa kweli. Kama ilivyo katika maono ya Ezekieli ya mifupa mikavu kurudi kuwa hai tena, watu hawa watatoka makaburini mwao na kuanza kumjua Mungu wao. Vitabu {yaani **“Biblia”** kwa lugha ya Kigiriki, ambayo imenakiliwa katika Kiswahili jinsi ilivyo bila kufasiriwa} ni maandiko, ambayo ndiyo chanzo pekee cha ufahamu wa uzima wa milele. Mwishowe wote watakuwa na nafasi kamili ya kufahamu mpango wa Mungu wa wokovu na uzima wa milele kwa ajili yao.

Ufufuo huu wa pili ulio wa kimwili si nafasi ya pili ya wokovu. Kwa watu hao watakaofufuliwa ni nafasi ya kwanza kwao ya kumjua Muumbaji. Watu hao waliofufuliwa **“wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao” {mstari wa 12}**. Hukumu hii itafanyika pindi ambapo watu hao watakuwa wamekwisha kupata nafasi ya kusikia, kufahamu na kukua katika njia ya uzima ya Mungu, na majina yao yakiwa yameandikwa katika kitabu cha uzima {mstari wa 15}. Katika kipindi hicho mamilioni na maelfu ya watu watapata nafasi ya kuingia katika uzima wa milele.

Msimu huu wa mwisho wa wokovu wa ulimwengu {yaani awamu ya tatu ya wokovu} unaonesha wingi wa utajiri wa rehema ya hukumu ya Mungu. Yesu Kristo alizungumzia uzuri wa pekee unaoashiriwa na awamu hii ya tatu ya wokovu pale alipoilinganisha miji mitatu ya Israeli na ile miji mingine mitatu ya Mataifa; **“Ole wako, Korazini! Ole wako, Bethsaida! Kwa kuwa kama miujiza iliyofanyika kwenu ingalifanyika katika Tiro na Sidoni, wangelitubu zamani kwa kuva magunia na majivu. Walakini nawaambieni, itakuwa rahisi Tiro na Sidoni kustahimili adhabu zao siku ya hukumu kuliko ninyi. Nawe Kapernaumu, je! utakuzwa mpaka mbinguni? utashushwa mpaka kuzimu; kwa kuwa kama miujiza iliyofanyika kwako ingelifanyika katika Sodoma, ungalikuwapo mji huo hata leo. Walakini nawaambieni, itakuwa rahisi nchi ya Sodoma kustahimili adhabu yake siku ya hukumu kuliko wewe” Mathayo 11:21-24.**

Wakazi wa Tiro, Sidoni na Sodoma, miji ambayo iliangukiwa na hasira ya Mungu, watapata rehema katika siku ya hukumu. Hali kadhalika Korazini, Bethsaida na Kapernaumu, miji hii ya zamani ilikuwa na nafasi ndogo ya kumjua Mungu. Mungu atawafufua watu hao na kuwajumuisha katika kipindi cha hukumu kilichopo baada ya miaka 1,000 ya utawala wa Kristo, wakati ambapo wote walioishi katika giza na ujinga watapatanishwa na Mungu. Utakuwa ni wakati wa kila mtu kumjua Mungu. Tangu wadogo hadi wakubwa, wote watamjua {soma **Waebrania 8:11**}. Wakazi wa miji hiyo, pamoja na mingine zaidi kama hiyo ambayo haikutajwa hapa, watapewa nafasi yao kwa ajili ya wokovu.

Kipindi hiki cha mwisho cha hukumu kinakamilisha mpango wa Mungu wa wokovu wa ulimwengu. Kitakuwa ni kipindi cha upendo, rehema nyingi na hukumu ya haki ya Mungu. Nafasi ya kunywa maji ya uzima ya Roho Mtakatifu itakuwa imepatikana na kuzima kiu ya wanaume na wanawake. Kipindi hiki cha hukumu ya haki kitawaleta kuwa hai wote ambao walikwisha sahauliwa na wanadamu, lakini hawakusahauliwa na Mungu.

Je; ni nini hatima ya wote wafao pasipo ufahamu wa kweli wa Yesu Kristo, mwana wa Mungu? Kuna tumaini gani kwa mamilioni ya watu walioishi na kufa pasipo kufahamu makusudi ya Mungu? Maandiko yameonesha kuwa hawakutupwa mbali bila matumaini. Mungu atawafufua na kuwapa nafasi kwa ajili ya wokovu wa milele. Mungu ataukamilisha mpango wake wa kuwaleta wana wengi waufikilie utukufu {soma **Waebrania 2:10**}. Ahadi yake aliyoahidi akisema, **“nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili”** itatimizwa {**Yoeli 2:28**}. Kiu ya Roho Mtakatifu itapozwa kwa wote katika kipindi hiki cha awamu ya tatu na ya mwisho katika mpango wa wokovu wa ulimwengu. Naam; kipindi hiki cha awamu ya tatu ya wokovu kitachukua muda wa miaka mia moja {soma **Isaya 65:20**}.

Wapendwa; ni mpango wa ajabu kiasi gani unaotangazwa na Injili ya Yesu Kristo; yaani Habari Njema ya Ujio wa Ufalme wa Mbinguni hapa Duniani *{Soma Marko 1:14-15}*! Ni mpango uliojaa wingi wa neema, rehema na upendo usio na kifani kwa wanadamu wote bila kusahauliwa mtu awaye yote! Naam; hii ndiyo Injili aliyoihubiri Yesu Kristo pamoja na Mitume wake; tena ilihubiriwa na Manabii wa Mungu tangu zamani kama tulivyojifunza. Naam; Injili hii inaendelea kuhubiriwa na Kanisa hili la Mungu hadi mwisho kama lilivyoagizwa na Yesu Kristo mwenyewe *{soma Mathayo 10:7-9; 24:14; 28:19-20}*.

Ni nini hatima ya wote wanaokataa kutubu?

Japokuwa Mungu atatoa nafasi kubwa sana ya wokovu kwa wote ambao hawakumjua, lakini baadhi yao watakataa kutubu, wala kujinyenyekeza kwa Mungu ili wapokee zawadi yake ya uzima wa milele. Sasa basi; ni nini hatima yao? Biblia inafunua wazi kwamba, watu hao hawataendelea kuishi huku wakiteseka kwa kuungua ndani ya moto milele kama wengi wanavyofundisha; bali wataangamizwa kabisa na kuwa kana kwamba hawakuwahi kuwapo kabisa! *Ufunuo 20:15* inatuambia kuwa, baada ya hukumu ya mwisho ya awamu ya tatu ya wokovu, *“iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto”* Na *Ufunuo 21:8* inaongeza kusema; *“Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili”*.

Ileleweke hapa vizuri, kwamba hatima yao ni mauti na wala si kuendelea kuishi ndani ya moto huo milele kwa maumivu mengi! Paulo pia alifahamu kuwa mwisho wa waovu ni mauti, na akasema; *“Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu” Warumi 6:23*. Hapa anabainisha wazi kwamba kuendelea kung’ang’ania dhambi zetu, mwisho wake ni mauti; na kukubali kutakaswa na kafara ya Kristo iliyotolewa kwa ajili yetu, ni kupata uzima wa milele.

Naye nabii Malaki anaweka wazi hatima ya waovu wote akisema; *“Kwa maana, angalieni, siku ile inakuja, inawaka kama tanuru; na watu wote wenye kiburi, nao wote watendao uovu, watakuwa makapi; na siku ile inayokuja itawateketeza, asema BWANA wa majeshi; hata haitawaachia shina wala tawi”*

“Lakini kwenu ninyi mnaolicha jina langu, jua la haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa zake; nanyi mtatoka nje, na kuchezecheza kama ndama wa mazizini. Nanyi mtawakanyaga waovu; maana watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu; katika siku ile niifanyayo, asema BWANA wa majeshi” Malaki 4:1-3.

Wapendwa; Mungu wetu ni mwenye upendo na rehema nyingi sana, na kamwe hapendi kuwatesa wanadamu wala kuwaua *{soma Maombolezo 3:33; Ezekieli 18:23,30-32}*; na hivyo basi hawezi kuvumilia kuona wanadamu aliowaumba kwa mfano wake, japokuwa wamemkataa, wakiendelea kuteseka ndani ya moto kwa maumivu ya milele! Na badala yake, moto utawateketeza mara moja, na kugeuka makapi na majivu, wasiwepo tena kabisa milele. Mungu wetu ni Mungu mwenye huruma na rehema ajabu!

Mafundisho ya kwamba waovu watateswa milele na milele katika moto ni mafundisho ya uongo na mapokeo ya wanadamu na wala si mafundisho ya kweli ya Biblia *{Kwa maelezo ya kina zaidi kuhusu jambo hili, agiza kitabu chetu kisemacho, “KIFO NA KIYAMA”, ili ujifunze zaidi, na utatumiwa bure}*.

Sura ya sita

YERUSALEMU MPYA

Mara baada ya mambo hayo yote kutimia kama yalivyokusudiwa na Mungu tangu mwanzo; yaani baada ya Kristo Yesu kumaliza kazi yake yote aliyopewa na Mungu Baba ya kuwapatanisha wanadamu na Mungu wao kama tulivyoona, pamoja na kumlipa kila mtu kwa kadiri ya maamuzi {au uchaguzi/matendo} yake {soma Yohana 3:16-17; 5:30; 17:2-8; Ufunuo 20:13; 22:12}; ndipo Biblia inatuambia jambo lingine litakalofuata ikisema; **“Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena. Nami nikaona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe. Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu {Baba} mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita. Na yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi akasema, Tazama, nayafanya yote kuwa mapya. Akaniambia, Imekwisha kuwa. Mimi ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho. Mimi nitampa yeye mwenye kiu ya chemhemi ya maji ya uzima, bure. Yeye ashindaye atayarithi haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu”.** Ufunuo 21:1-7. Tafadhali soma kuendelea katika sura hii yote ya **ufunuo 21** hadi ule mstari wa 27 ili upate picha angalahu kidogo kuhusu huo mji mtakatifu, yaani Yerusalemu mpya!

Naam; kupitia kwa Yesu Kristo, tutaweza kumuona na kuishi pamoja na Mungu Baba yetu ambaye kabla ya hapo, hakuna ye yote aliyewahi kumuona wala kumsikia sauti yake isipokuwa tu kwa kupitia kwa Yesu {soma Yohana 5:37}. Hii ina maana kwamba, hakuna mwenye dhambi awaye yote atakayemuona wala kumsikia Mungu Baba isipokuwa watakatifu pekee, maana wakati huo tayari wenye dhambi {yaani waovu wote} watakuwa wamekwisha kuangamia kabisa {soma **Waebrania 12:14**}.

Wapendwa; hivyo ndivyo mambo yalivyo na ndiyo ukweli pekee wa Biblia, ikitueleza tangu mwanzo wa kuumbwa kwa Sayari hii Dunia, hadi kufikia mwisho wake. Na tena Biblia ikitueleza mpango kamili wa Mungu kwa Wanadamu wote chini ya mbingu. Na mambo haya kwa sasa ni siri ya Mungu iliyofichwa kwa ulimwengu wote {soma **Mathayo 11:25-26**}; lakini yamefunuliwa kwetu sisi kwa neema ya Mungu mwenyewe kama Maandiko haya yasemavyo kwamba; **“Lakini, kama ilivyoandikwa, Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu. Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu. Lakini sisi hatukupokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu. Nayo twayanena, si kwa mameno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyaifasiri mambo ya rohoni kwa mameno ya rohoni”.** 1 Wakorintho 2:9-13. Soma pia **Mathayo 13:10-16**.

Sura ya saba

VIPI KUHUSU KWENDA MBINGUNI?

Dhana dhidi ya ukweli

Tafadhali liweke jambo hili kichwani kwamba, **“hakuna unabii katika maandiko {katika Biblia} upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu” 2 Petro 1:20-21.**

Je! hili linamaanisha kwamba wanadamu hawawezi kuyafahamu maandiko? Wapendwa; jihadharini na manabii wa uongo ambao wanalitumia andiko hili vibaya kwa kisingizio cha kiroho na hivyo kupotoa ukweli wa maandiko. Kwa mujibu wao, neno la Mungu {unabii} ni lugha yenye kubadilika maana yake pale inapokuja katika maandiko. Fahamuni basi ya kwamba, lugha ni njia ya mawasiliano yenye kufikisha kile kinachomaanishwa.

Sasa basi; ni nini roho ya maandiko ambayo ndiyo pekee iwezayo kuyafafanua katika hali iyo hiyo ya kiroho? Yesu Kristo alilifahamu hili vizuri sana na wala hakuliacha pasipo kulitolea ufafanuzi.

Biblia ni kitabu kilichoandikwa na watu tofauti-tofauti na kwa nyakati tofauti-tofauti pia. Uandishi wake ulichukua mlolongo mrefu kuanzia pale katika Mlima Sinai hadi katika siku za Yohana wa ufunuo. Kwa hivyo, hali ya kiroho ni hii kwamba, hakuna mstari {au kifungu} mmoja unaokamilisha jambo. Kwa maana kwamba, hatuwezi kutumia mstari ama kifungu kimoja kuelezea au kufafanua mada. Mistari ya Biblia ni kama fumbo au chemshabongo inayohitaji kujazwa ili kuleta maana kamili ya jambo. Yesu, ambaye ndiye pekee awezaye kuifungua ametoa muongozo wa namna ya kuijaza. Watu wengi wamedanganyika na kuudharau huo muongozo, na hivyo kuwa na dhana {mawazo ama fikira binafsi, kuwazia wenyewe} nyingi dhidi ya maandiko na kufanya mstari mmoja kuwa na maana nyingi tofauti-tofauti kama vile dhana zilivyo nyingi na tofauti pia.

Yesu Kristo anasema hivi kuhusu namna iliyo sahihi na kweli ya kujifunza katika ufahamu wa kiroho. Tafadhali lifahamuni jambo hili wapendwa; **“Atamfundisha nani maarifa? atamfahamisha nani habari hii?...Kwa maana ni amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo” Isaya 28:9-10.** Tuko hapo wapendwa? Yesu anasema; **“Mwapotea, kwa kuwa hamyajui maandiko wala uweza wa Mungu” Mathayo 22:29.** Sababu ya kutoyafahamu maandiko ni hii; kwanza, watu wameukataa na kuutupilia mbali huo muongozo wa kujifunza biblia. Na jambo la pili; watu hawajipatii muda wa kutosha wa kujifunza biblia.

Hivyo basi; kwa kuelewa mafungu machache, na wakati huo huo wakijaribu kuwa waalimu, wanachofanya ni kukamilisha yale wasiyoyaelewa kwa mawazo {dhana/fikira} yao wenyewe ambayo yanatokana na nia ama akili ya kimwili na kuyachanganya na maandiko na hivyo kulazimika kuongeza ama kupunguza neno la Mungu; na hili ni jambo ambalo Mungu amekataza {soma Mithali 30:5-6; Ufunuo 22:18-19}.

Hizi dhana zinazoongezwa katika maandiko zenye kutokana na ufahamu wa kimwili ndizo chanzo cha maelfu ya makundi ya Kikristo leo. Lakini, ijapokuwa ni makundi mengi sana, yote yana jambo moja ambalo ni asili yao. Ni jambo gani? Wanaikataa amri {maandiko} ya Mungu ili wapate kuyashika mapokea {dhana, fikira, mawazo} yao {soma Marko 7:9}. Wanayakataa baadhi ya maandiko na huku mengine wakiyapotoa. Kwa hivyo, wajapokuwa makundi mengi, wote wanajifunza kutoka kwa mwalimu mmoja, na hivyo wao ni kitu kimoja; yaani ni **“Sinagogi la**

Shetani” Ufunuo 3:9. Pia wanajumuika katika yule roho mmoja, yaani Babeli {*mkanganyiko au machafuko*}, ambaye Mungu anawaambia wote wale waijuao sauti ya mchungaji wao, Yesu Kristo, kwamba ***“Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake”*** Ufunuo 18:4.

Mfano hai

Karibu wote wanaoamini katika kile kinachoitwa Ukristo leo, wanaamini kwamba Kristo atarudi duniani kuwachukua waaminio {*yaani watakatifu*} na kuwapeleka mbinguni ambako wataishi huko maisha ya furaha milele na milele. Na ukijaribu kumuuliza ye yote kati yao kwamba ni wapi wanapolisoma jambo hili katika biblia; basi atakupeleka haraka sana katika kitabu cha ***Yohana 14:1-3.*** Swali la msingi ni hili; je, mafungu {*mistari*} hayo ya maandiko yanazungumzia ama kuashiria cho chote kuhusu kwenda mbinguni? Kwa hakika hapana; na hili liko wazi kabisa, maana imeandikwa; ***“Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo”*** ***Yohana 14:1-3.*** Sasa basi; ni wapi hapo atakapokuwapo Yesu ambako nasi tutakuwapo? Wapendwa; endapo mtu atatumia mafungu haya-haya kujaribu kujibu swali hili; basi kile atakachofanya ni kudhania tu kwa fikira zake mwenyewe, maana mafungu haya hayakusema ni wapi! Kwa hivyo wote wanaotumia mafungu haya kama kigezo cha uthibitisho wa kwenda mbinguni wanadhania tu kwa mawazo yao. Maandiko hayo yameishia kwa ufupi tu bila kusema ni wapi!

Hivyo basi; hebu tufuatilie kanuni ya kifungu juu ya kifungu; huku kidogo na huku kidogo {*Isaya 28:10*} ili tufahamu ni wapi Kristo atakapokuwapo pamoja na watakatifu. Sikia vile kifungu kingine kisemavyo; ***“Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki {yaani, tumpokee} Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele”*** ***1 Wathesalonike 4:16-17.*** Ndiyo; mafungu haya yanaonesha vema kwamba atakapokuja Kristo tutamlaki {*tafakari kwa makini maana ya neno “kulaki” au “kupokea”*} hewani {*ama mawinguni*} na kisha tutakuwa pamoja naye milele. Je! umesikia kwamba tutakuwa pamoja naye milele wapi? Je! ni mbinguni; au je, ni hapo-hapo hewani; ama je, ni mahali fulani? Kwa hakika maandiko haya hayo hayakusema ni wapi tutakapokuwa pamoja na Kristo baada ya kumpokea hewani!

Kwa hivyo basi, bado tunajiuliza; ni wapi tutakapokuwapo? Sikia basi jinsi maandiko mengine yasemavyo kwamba; ***“Tazama, siku moja ya BWANA inakuja,...Na siku hiyo miguu yake itasimama juu ya mlima wa Mizeituni, unaoelekea Yerusalemu upande wa mashariki,...”*** ***Zakaria 14:1,4.*** Tunaamini kwamba kufikia hapo ndugu msomaji, umeanza kuona jinsi ambavyo Biblia inajieleza {*inajifafanua*} yenyewe bila shida kabisa. Iko wazi hapa kwamba, kutoka pale hewani, Kristo pamoja na Watakatifu hawatakwenda mbinguni, na badala yake, watateremka chini hadi kufika juu ya mlima wa Mizeituni ambao unafahamika pia kama mlima Sayuni. Ni mlima ule-ule ambao wakati wa kwenda kwake mbinguni baada ya kufufuka, Yesu Kristo alichukuliwa kutoka juu yake; naam, ni mahali hapo-hapo ndipo wakati wa kurudi kwake pia atateremkia {*soma Matendo 1:9-12*}

Na kufikia hapo, ahadi ya Mungu itatimizwa; ahadi ile isemayo; ***“Na ufalme, na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote {sio juu mbinguni}, watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu; ufalme wake ni ufalme wa milele, na wote wenye mamlaka {yaani, watawala wa ulimwengu huu wa sasa} watamtumikia na kumtii”*** ***“Naye BWANA atakuwa mfalme juu ya nchi {sio juu ya mbingu} yote; siku hiyo BWANA atakuwa mmoja, na jina lake moja”*** ***Danieli 7:27; Zakaria 14:9.***

Wapendwa; kufikia hapa ndipo tunaweza kufahamu kile kilichomaanishwa katika *Yohana 14:1-3*. Ni katika Dunia hii hii ufalme wa Mungu utakuja, na ndipo Kristo na Watakatifu watakapokuwapo wakitawala. Hii ndiyo maana Kristo anatuambia tuombe kwamba, **“Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni”** *Mathayo 6:9-10*. Naye Kristo kwa damu yake mwenyewe anawakomboa watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa ili awafanye **“kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; {kisha watu hao wafanye nini?} nao wanamiliki juu ya nchi {sio mbinguni}”** *Ufunuo 5:9-10*.

Je! watakatifu wanaokufa wanakwenda mbinguni?

Kutokana na mawazo ya watu kujazwa na dhana ya kwamba tutakwenda kuishi mbinguni milele, huku mawazo na dhana hizo zikiwa ni kinyume kabisa na maandiko na mpango wa Mungu kwa wanadamu; basi kumetokea mkanganyiko na kutokubaliana kuhusu ni jinsi gani ama ni kwa njia gani watu wanakwenda ama watakwenda huko mbinguni. Wapo wale wanaodai kwamba, iwapo mtu amekuwa mcha Mungu wa kweli; basi pindi tu mauti inapomfika, mtu huyo uenda moja kwa moja hadi juu mbinguni kwa Mungu na kuanza kuishi maisha ya raha mustarehe huko mbinguni, huku akifanya kazi moja tu ya kuimba na kumtukuza Mungu. Tena wanadai kwamba, mtu mwovu naye pindi anapokufa tu, hupelekwa moja kwa moja Jehanamu *{yaani katika ziwa la moto}* kwenda kuteswa kwa maumivu ya moto milele pasipo kufa! Jambo la kushangaza ni kwamba, watu hao wenye imani hiyo, wakati mwingine tena utawasikia wakisema eti Yesu Kristo atakapokuja atawafufua wafu! Sasa tujiulize sote; ikiwa wacha Mungu wanaokufa tayari wanakwenda mbinguni punde tu wanapofariki; je! huyo Yesu anakuja kuwafufua akina nani wakati watakatifu wake amewaacha mbinguni, huku pia waovu ameishawatupa motoni na wanaendelea kuteseka? Kwa maana nyingine ni kusema kwamba pindi tu mtu anapokufa, awe mwema ama mwovu, hupokea ujira wake kutoka kwa Mungu, jambo ambalo ni kinyume cha mafundisho ya biblia *{soma Mithali 12:14; Isaya 40:10; 62:11; Ufunuo 22:12}*.

Wapendwa; jihadharini na manabii wa uongo na mafundisho ya kishetani. Biblia inatuambia kwamba; **“Maana mautini hapana kumbukumbu lako; Katika kuzimu ni nani atakayekushukuru?”** Tena inasema; **“Sio wafu wamsifuo Bwana, wala wo wote washukao kwenye kimya”** *Zaburi 6:5; 115:17*. Na kwa kuyathibitisha maandiko haya; Yesu Kristo aliyekuja duniani akitokea mbinguni baada ya watakatifu wa Mungu wengi kufariki, alituambia kwamba; **“Wala hakuna mtu aliyepaa mbinguni, ila yeye aliyeshuka kutoka mbinguni, yaani, Mwana wa Adamu”** *Yohana 3:13*. Wapendwa; mtamwamini Yesu Kristo aliyeshuka kutoka mbinguni na neno lake la kweli ama mtaendelea kuyaamini na kuyashika mafundisho na mapokeo ya wanadamu? *{soma Marko 7:6-9}*.

Baada ya Kristo kuondoka; Mitume wake ambao ni miongoni mwa watakatifu tunaowanena, waliendelea kuthibitisha kwamba, hakuna mtu awaye yote aliyekwenda mbinguni akiwa hai ama baada ya kufariki. Mtume Petro anatuambia hivi; **“Waume, ndugu zangu, mniwie radhi, niseme kwa ujasiri mbele yenu habari za baba yetu mkuu, Daudi, ya kuwa alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo...Maana Daudi hakupanda mbinguni...”** *Matendo 2:29,34*. Naam, wapendwa; Watakatifu ni akina nani kama si hao akina Daudi ambao Biblia inasema wazi kwamba hawakwenda mbinguni? Kitabu cha *Waebrania 11* kinazungumza habari za hao Watakatifu wote na kinahitimisha kwa kusema; **“Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi; kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi”** *Waebrania 11:39-40*. Naam; Watakatifu wote wanangoja ufufuo pindi tu Kristo atakaporejea kwa mara ya pili tunakokutazamia hivi sasa *{soma 1 Wakorintho 15:50-52; 1 Wathesalonike 4:16-17}*, na wala hawako mbinguni! *{Kwa maelezo ya kina zaidi kuhusu habari za mauti, wafu na ufufuo; agiza kitabu chetu kisemacho, “KIFO NA KIYAMA”, kwa msaada zaidi na utatumiwa bure pasipo malipo}*.

Hitimisho

Wapendwa; ni kwa namna hii unaweza kujifunza na kuielewa Biblia kwa kanuni ya kiroho na hivyo kujiweka kando kabisa na mkanganyiko na machafuko yaliyomo ulimwenguni yatokanayo na dhana au fikira na mawazo ya watu ambayo misingi yake ni Shetani.

Kanisa la kweli la Mungu ambalo Kristo alilianzisha mwenyewe, ambalo alisema litadumu hadi wakati wa kurudi kwake *{soma Mathayo 16:18}*; na ambalo ndilo peke yake limepewa kuzijua siri za ufalme *{soma Mathayo 13:11}*; na ambalo ndilo pekee lililotumwa kuhubiri na kufundisha Biblia *{soma Mathayo 28:18-19}*; tena ambalo ndilo pekee liwezalo kukulisha kweli yote katika ukamilifu na kukufanya kuufikia “*umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu*” *{soma Waefeso 4:11-14}*; naam, liko hapa sasa kwa ajili yako. Lakini ni juu yako kuamua. Hii ni sauti ya Mchungaji wa kweli Yesu Kristo, anawaita walio wake hivi sasa, yaani wale waliokusudiwa wokovu katika awamu hii ya kwanza. Je! utaitikia wito wake leo?

Na kama utapenda kufahamu mengi zaidi katika mafundisho ya kweli ya Biblia; tunavyo vitabu vingine vingi kwa ajili yako vitolewavyo bure kabisa pasipo malipo, vitakavyokujulisha kweli na siri hizo za Biblia. Tunavyo vitabu kama vile; “**KIFO NAKIYAMA**”, ni kitabu kitakachokufahamisha habari za mauti, wafu na ufufuo wa wafu kama yasemavyo maandiko matakatifu ya Mungu.

Tuna “**KUFA NAKUFUFUKA KWA YESU KRISTO**”, ni kitabu kitakachokufahamisha ni lini alikufa na kufufuka Yesu Kristo kama vile yasemavyo maandiko *{biblia}* maana Yesu Kristo hakufa siku ya Ijumaa na wala hakufufuka siku ya Jumapili!

Tuna “**DINI ZA MITINDO**”, ni kitabu kitakachokufahamisha mambo yasiyofaa katika maisha ya Mkristo wa kweli pamoja na yale yafaayo yatakayokuwezesha kubadilika na kuelekea katika utakatifu na ukamilifu.

Tuna “**AMRI KUMI**”, hiki pia kitakufahamisha ni nini maana ya amri hizo, na zipo kwa ajili ya akina nani, na ikiwa ni muhimu katika maisha yetu leo kuzishika au la.

Tuna “**BIBLIA NA AFYA ZETU**”, hiki pia kitakufahamisha ni kitu gani Mungu anatuambia kuhusu vitu vile tunavyopaswa kula na kunywa pamoja na vile tusivyopaswa kuvitumia; au ikiwa Mungu ametuacha huru katika hili kwamba kila mtu na atende kama apendavyo mwenyewe au la.

Tuna “**SIKUKUU ZA MUNGU**”, kitabu hiki kitakufahamisha sikukuu za Mungu katika biblia, maana zake na umuhimu wa siku hizi katika maisha ya imani ya Ukristo; na pia kitakujulisha sikukuu za kipagani zilizopewa majina ya Ukristo na zinaadhimishwa na wale wajiitao kuwa Wakristo pasipokujua kwamba wanamfanyia Shetani ibada na si Mungu kama wanavyodhani kufanya.

Vitabu hivi pamoja na vingine vingi vitatolewa bure kwako pasipo malipo yo yote yale kutoka kwako. Unachopaswa kufanya ni kuagiza tu kile ama vile unavyovihitaji; na utupatie anuani yako kwamba ni jinsi gani vitakufikia hapo ulipo kwa urahisi na uhakika. Nasi pia bila hiyana kabisa tutahakikisha unapata kile unachokihitaji kutoka kwetu.

Wasiliana nasi kwa anuani zifuatazo:-

KANISA LA MUNGU – TANZANIA

Nambari za simu ni; +255 753 359 179, +255 688 359 179 na +255 655 659 179.

Barua pepe; Ukweliwabiblia@yahoo.com.sg

NA

KANISA LA MUNGU – KENYA

Barua pepe; endcog@gmail.com

*Neema na iwe kwenu na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu, na kwa Bwana wetu Yesu Kristo.
Utukufu una yeye tangu sasa na hata milele; Amina.*